

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

661

SAIKOLOJIA YA ELIMU NA KUNASIHI

Muda: Saa 3

Jumanne Novemba 02, 2004 Asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, maswali mawili (2) kutoka sehemu B na swali moja (1) kutoka sehemu C.
3. Simu za Mkononi haziruhusiwi katika chumba cha mtihani.
4. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu cha kujibia.

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

Swali la 1 lina alama 12, na mengine ni alama 3 kila moja.

1. Oanisha mawazo kutoka **ORODHA B** na yale yaliyoko kwenye **ORODHA A** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kando ya namba ya kipengele cha swali.

ORODHA A

- H (i) Mambo yanayoendelea na makuzi ya kimaono
D (ii) Hatua ya ukuaji inayoambatana na mabadiliko makubwa ya kimwili, kitabia, kiakili, kimaono na kijamii
A (iii) Kiwango cha hisa ya akili zaidi ya 139
B (iv) Kuathirika kiakili kunakosababisha akili ya mtoto kutoongezeka kulingana na umri wake wa kuzaliwa
C (v) Mtoto azaliwapo anaweza kurithi magonjwa kutoka kwa wazazi au vizazi vya wazazi wake
F (vi) Makuzi ya kimwili, kiakili, kimaono, kibaiba, kijamii na kitabia

ORODHA B

- A Mtoto mwenye uwezo unaohusiana na kiwango cha mwenye kipaji maalumu
B Kuvia akili
C Pumu, kifafa na kansa ya damu
D Kijana mwenye umri wa miaka 12 hadi balehe
E Mtoto mwenye uwezo unaohusiana na kiwango cha akili ya juu zaidi
F Aina za makuzi ya mtoto
G Mtu mzima mwenye umri wa miaka 25
H Kujenga woga, hasira, wivu, upendo, na msisimko
I Malaria, kuhara damu
J kipindupindu
K Makuzi ya kimwili
L Mtoto
M Mama mjamzito

2. Fafanua kwa ufupi kanuni ya matokeo katika kujifunza.

3. Andika vipindi vitatu (3) vya mazingira ya ukuaji wa mtoto

4. Nini maana ya haiba kisaikolojia? *mwenekano wa ndani na nje ya mtoto*

5. Andika mambo matatu (3) yanayoweza kusababisha mwanafunzi kukumbuka mambo aliyofundishwa.

6. Eleza tofauti iliyopo kati ya motisho-shauku na motisho-kishawishi. *Mwanafunzi kutokana na mtoto aliyofundishwa*

7. Andika nyanja tatu (3) za malengo ya kielimu kama zilivyobainishwa na mtaalamu Bloom (1959). *Stadi, Maanifa, Muelekeo*

8. Bainisha aina tatu (3) za kujifunza. *Kuiga, kutanini, kuinganua*

9. Fafanua na eleza kwa ufupi aina tatu (3) za uhawilishaji mafunzo. *Uhawilishaji changa*

12
Shauku ni matakama ulio ndani ya mtoto
Shawishi " " nje " "

SHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali mawili (2) katika sehemu hii

10. Eleza njia tatu (3) zinazoweza kutumiwa katika kutoa ushauri kwa mtu au watu.
11. Eleza matokeo sita (6) ya mabadiliko ya kukua yajitokezayo wakati kijana anapofikia hatua ya kubalehe.
12. (a) Nini maana ya kusahau?
(b) Katika hali ya kufundisha na kujifunza, eleza njia za kuweza kupunguza kasi ya mwanafunzi kusahau mambo aliyofundishwa.
13. Eleza sifa nne (4) ambazo mtoto wa miaka 6 hadi 11 anakuwa nazo, na ambazo humtofautisha yeye na mtoto wa miaka 2 hadi 5.

SEHEMU C (Alama 24)

Jibu swali moja (1) katika sehemu hii.

14. (a) Nini maana ya madawa ya kulevyu?
(b) Eleza mambo tisa (9) ambayo yakitekelezwa kikamilifu yanaweza kupunguza au kuondoa tatizo la utumiaji madawa ya kulevyu nchini Tanzania.
15. (a) Nini maana ya adhabu?
(b) "Utoaji wa adhabu kwa wanafunzi katika mazingira ya kufundisha na kujifunza una dosari". Eleza dosari hizo na pendekeza njia mbadala ambazo ni sahihi kuzitumia katika mazingira hayo.
16. Eleza umuhimu wa kutoa ushauri nasaha kwa wanafunzi wa shule ya msingi, hususan wale wenye matatizo ya kielimu na kifamilia.

ushirikiano wakati wa kufunza

Kufanya kwa vitendo ✓
Mwali mu kutumia njia shi ✓
matumizi mazuri ya ranga ✓
mwali maswali na majibu ✓

Kuwa pa mazoezi, majaribu ✓
Kuwa pa matisho

Mwali mu mwenye taaluma ✓ Kumbanani
matibabu

Kuamini vifanya

Kutoa ajira

Kutoa kumpuni ✓

Kuweka sheria